

HALMASHAURI YA MJI WA KONDOA

(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Halmashauri ya Mji wa Kondoa)

MJI WA KONDOA
Simu: +255 262360028
Fax: +255 262360028
Barua pepe :td@kondoatc.go.tz



Mkurugenzi wa Mji
Sanduku la Posta 711,
KONDOA.

TANGAZO LA KAZI

01/01/2018

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kondoa anawatangazia Wananchi wote wenye sifa ambao ni raia wa Tanzania kuomba nafasi za kazi za Mkataba kama ifuatavyo:-

1. Dereva nafasi:Saba (7)

- **Sifa za Mwombaji**
 - ❖ Awe raia wa Tanzania
 - ❖ Awe na Elimu ya KIdato cha Nne (IV)
 - ❖ Awe na Leseni ya Udereva katika Daraja E au C ya uendeshaji magari na ameendesha gari kwa kipindi cha mwaka mmoja (1) bila kusababisha ajali
 - ❖ Awe amehudhuria mafunzo ya Uendeshaji wa Magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha Ufundı Stadi (VETA), Chuo cha Usafirishaji cha Taifa (NIT) au chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.
 - ❖ Mwenye cheti cha Majoribio ya Ufundı Daraja la Pili II watafikiriwa kwanza.

2. Kazi na Majukumu

- ❖ Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari.
- ❖ Kupeleka watumishi maeneo mbalimbali ya safari.
- ❖ Kufanya matengenezo madogo ya gari
- ❖ Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali
- ❖ Kujaza na kutunza nyaraka za safari zote katika daftari la safari
- ❖ Kufanya usafi wa Gari.
- ❖ Kufanya kazi nyingine kadri atakavyo elekezwa na msimamizi wake.

3. Mshahara.

❖ Mshahara ni Tshs 250,000/= kwa mwezi.

4. Masharti ya Ajira.

Ajira itakuwa ya Mkataba wa Miezi Mitatu baada ya hapo kama kutakuwa na uhitaji taratibu zingine zitafanyika.

5. Namna ya Kutuma maombi.

Maombi ya kazi yaambatane na nakala ya vyeti vifuatavyo; -

- v. Cheti cha kidato cha Nne au Sita
- vi. Vyeti vya taaluma
- vii. Cheti cha Kuzaliwa
- viii. Wasifu CV iliyobandikwa picha ya bluu.

6. Mwisho wa kutuma maombi.

Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 14/01/2019 saa 09:30 Alasiri.

7. Barua ya maombi iandikwe kwa Mkono na itumwe kwa njia ya Posta kwa anuani ifuatayo; -

**MKURUGENZI,
HALMASHAURI YA MJI,
S.L.P 711,
KONDOA.**

TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA;-


**Msoleni J. Dakawa
MKURUGENZI MJI
KONDOA**



Nakala;- Mbao za Matangazo.
KONDOA.